

**MAELEZO YA MKURUGENZI MKUU WA TAKUKURU
BRIGEDIA JENERALI JOHN JULIUS MBUNGO WAKATI WA
HAFLA YA UZINDUZI WA OFISI SABA ZA TAKUKURU
WILAYA PAMOJA NA JENGO LA OFISI YA INTELIJENSIA
CHAMWINO - DODOMA**

JULAI 22, 2020

Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Mama Samia Suluhu Hassan

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Kasim Majaliwa Majaliwa

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Job Ndugai

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano

Mhe. George Simbachawene

Waziri wa Mambo ya Ndani – ambaye anamwakilisha Waziri wetu **Mhe. Kapt. Mstaafu George Mkuchika**, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Dkt Binilith Mahenge

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;

Viongozi wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wakiongozwa na
CDF Venance Mabeyo

Wakuu wa Idara wa Taasisi za Umma na Binafsi mlioko hapa,

Viongozi wa Dini,

Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Watumishi wenzangu wa TAKUKURU;

Waandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana

Asalaam Aleykum,

Tumsifu Yesu kristu.

Mheshimiwa Rais,

SHUKRANI:

Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa huruma na upendo kwa kukujalia wewe **Mheshimiwa Rais** afya njema ya mwili na roho, lakini pia kwa kutu kutanisha sisi sote hapa siku hii ya leo tukiwa na afya njema wote, huku tukifurahia Amani, Utulivu na Maendeleo ya nchi yetu ambayo wewe **Mheshimiwa Rais**, ndiye Mratibu Mkuu.

Mheshimiwa Rais,

Kwa namna ya kipekee kabisa, ninapenda kuchukua fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi kwa kuridhia ombi letu la kuwa Mgeni Rasmi. Pia ninakushukuru kwa kutenga muda wako adhimu na kukubali kufanya shughuli hii ya uzinduzi wa majengo ya ofisi yaliyojengwa kwenye wilaya saba pamoja na Jengo la ofisi ya Intelijensia lililopo Dodoma Mjini.

Majengo hayo yote yanazinduliwa rasmi leo siku ya Jumatano, Julai 22, 2020 kwa uzinduzi utakaoufanya kwenye Jengo hili la ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Chamwino. **TUNAKUSHUKURU SANA MHESHIMIWA RAIS!**

Mheshimiwa Rais,

Kama nilivyoeleza hapo awali, leo utatuzindulia jumla ya majengo ya ofisi saba za TAKUKURU ngazi ya wilaya pamoja na jengo la Intelijensia lililopo Dodoma mjini. Majengo husika ambayo yatazinduliwa kwa kuwakilishwa na jengo hili la TAKUKURU Wilaya ya Chamwino ni haya yafuatayo:

1. Jengo la TAKUKURU Wilaya ya Mwapwa mkoani Dodoma
2. Jengo la TAKUKURU Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha
3. Jengo la TAKUKURU Wilaya ya Manyoni mkoani Singida
4. Jengo la TAKUKURU Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara
5. Jengo la TAKUKURU Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma
6. Jengo la TAKUKURU Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi **na mwisho ni**
7. Jengo la Ofisi za Intelijensia lililoko hapa Dodoma

MHESHIMIWA RAIS TUNAKUSHUKURU SANA!!

Mheshimiwa Rais,

Kwa kutambua umuhimu wa TAKUKURU kuwa na majengo yake ya ofisi ambayo ni ya kisasa na ya kudumu na ambayo yanajitegemea, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2017/ 2018, ulitupatia jumla ya shilingi **Bilioni 1**, kwa ajili ya ujenzi wa majengo saba ya ofisi za TAKUKURU ngazi ya Wilaya.

Fedha hizo ndizo zilizofanikisha kujenga ofisi saba za TAKUKURU ngazi ya Wilaya nilizozitaja hivi punde, na ofisi hizo zimejengwa kwa mchoro wa aina moja unaofanana na jengo hili utakalo lizindua leo. **Mheshimiwa Rais**, picha za majengo yote ya TAKUKURU wilaya ambayo yatazinduliwa leo ni kama yanavyoonekana katika picha na mabango yaliyowekwa mbele yako.

Mheshimiwa Rais,

Majengo hayo yote, yamejengwa kwa kutumia njia ya manunuzi ya **'Force Account'** chini ya usimamizi wa wataalamu kutoka ndani ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na majengo haya yamejengwa kwa muda wa kati ya **miezi 7 hadi 12**.

Mheshimiwa Rais,

Ninayo furaha kukufahamisha kwamba ndani ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - TAKUKURU tunacho Kitengo cha Usimamizi wa Miliki na Mali, ambacho kazi yake kubwa ni kusimamia masuala ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi; Usimamizi na uthamini wa mali za Taasisi pamoja na ufundi kwa ujumla.

Mheshimiwa Rais,

Kitengo hiki kilishiriki kikamilifu katika ujenzi wa majengo haya ya Wilaya ambayo yote utayazindua leo hii.

Kupitia Kitengo hiki, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imefanikiwa kupunguza gharama za ujenzi wa miradi mbalimbali kwani kitengo hiki kina wataalam wenye fani za ujenzi wakiwamo wahandisi, wasanifu majengo, wakadiriaji majenzi na wathamini ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa majengo yanayojengwa kwa ajili ya TAKUKURU yanazingatia ubora na thamani ya fedha (Value for Money).

Mheshimiwa Rais,

Napenda kuwatambulisha kwako maafisa wa Kitengo cha Usimamizi wa Miliki na Mali tulionao leo hii, ambao wamekuwa wakinisaidia katika usimamizi wa ujenzi wa majengo yetu. Maafisa hao ni:

- Jarudi Nyakongeza (Msanifu wa Majengo – Architect)
 - Alvin Kiwia (Mkadiriaji wa Majenzi – Quantity Surveyor)
- pamoja na**
- Tito Johnson (Mthamini – Valuer)

Vilevile, ninaomba kwa heshima niwatambulishe kwako wataalamu walioshiriki katika usimamizi wa majengo haya ya TAKUKURU utakayoyazindua leo hii ambao ni:

- (i) Fortunatus Ngailo ambaye ni Msanifu wa Majengo (Upande wa Mshauri – Consultant) **pamoja na**
- (ii) Masoud Mtwale ambaye ni Mkadiriaji Majenzi – Quantity Surveyor (Upande wa Mjenzi)

TUNAKUSHUKURU SANA!

Mheshimiwa Rais,

Kwa kutambua kuwa mojawapo ya mbinu za kuzuia na kupambana na rushwa ni kuziimarisha na kuzijengea uwezo Taasisi zinazosimamia mapambano hayo na kwa kupitia dhamira yako ya kutaka kupambana na Rushwa kwa nguvu zako zote na katika nyanja zote, mara zote umekuwa ukihakikisha kwamba unaiimarisha Taasisi yetu ili iweze kutekeleza jukumu la kuongoza mapambano dhidi ya rushwa kwa umahiri na ufanisi - katika Taifa letu.

Ninakushukuru sana **Mheshimiwa Rais**, kwa kuiwezesha TAKUKURU kujenga majengo hayo yote pamoja na kutuwezesha kwa kutupatia vitendea kazi, rasilimali fedha na rasilimali watu - mambo ambayo umekuwa ukitupatia mara kwa mara kama ifuatavyo:

MUUNDO WA TAKUKURU:

Mheshimiwa Rais,

Ninakushukuru sana kwa kuruhusu Muundo wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kufanyiwa marekebisho mara mbili. Mara ya kwanza muundo huu ulifanyiwa marekebisho - **Agosti mwaka 2016** na mara ya pili ulifanyiwa marekebisho - **Novemba mwaka 2018.**

Katika marekebisho yaliyofanyika, pamoja na mambo mengine Muundo wa TAKUKURU ulirekebisha nafasi ya NAIBU MKURUGENZI MKUU WA TAKUKURU kwa kumuainishia majukumu yake ambayo yalikuwa hayatamkwi kabisa na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007 ambayo ndiyo inayoongoza chombo hiki.

Mheshimiwa Rais,

Jambo hili lilisababisha NAIBU MKURUGENZI MKUU WA TAKUKURU kutokuwa na majukumu ya kufanya, suala ambalo lilinipa 'Kigugumizi cha Kiutendaji' wakati uliponiteua kuwa NAIBU MKURUGENZI MKUU WA TAKUKURU mwaka **2017**.

Mheshimiwa Rais,

Mabadiliko haya kwetu sisi ni mafanikio makubwa na ninaamini kuwa NAIBU MKURUGENZI MKUU WA TAKUKURU atakayeteuliwa – ikikupendeza, hatakutana na kigugumizi cha kiutendaji kama ilivyonikuta mimi.

Mheshimiwa Rais,

Nichukue fursa hii pia kuwashukuru aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU wakati unaniteua - Mheshimiwa Balozi Valentino Mlowola, ambaye wakati mwingi alinituma kufuatilia na kusimamia maendeleo ya ujenzi wa majengo ya ofisi hizi za wilaya.

Vilevile, ninamshukuru Kamishna Diwani Athumani – aliyekuwa MKURUGENZI MKUU WA TAKUKURU baada ya Mheshimiwa Balozi Mlowola, ambaye naye alinituma sana kuja kukagua maendeleo ya ujenzi wa ofisi hizi.

Nadhani viongozi wote hawa wawili walitabiri au walikuwa na maono kuwa uzinduzi wa ofisi hizi na hususan ofisi hii ya TAKUKURU Wilaya ya Chamwino ungefanyikia hapa Chamwino tena chini ya usimamizi wangu mbele ya **Mheshimiwa Rais. WOTE KWA PAMOJA NINAWASHUKURU SANA!**

UTENDAJI KAZI WA TAKUKURU:

Mheshimiwa Rais,

Mafanikio ya utendaji kazi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa – TAKUKURU uliyaeleza vyema katika hotuba yako uliyoitoa Juni 16, 2020 wakati ukihitimisha Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapahapa Dodoma. Katika hotuba ile, **Mheshimiwa Rais** ulitumia takriban **dakika saba** kuelezea Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa pamoja na mafanikio yake.

Sikusudii kurudia tena kueleza mafanikio ya TAKUKURU bali nitumie fursa hii **kukushukuru** na **kukupongeza** sana kwa niaba ya watumishi wenzangu wa TAKUKURU na kuahidi mbele yako kwamba tutaendelea kuchapa kazi bila woga wala upendeleo katika vita hii dhidi ya rushwa ambayo TAKUKURU imepewa dhamana ya kuiongoza. **HONGERA SANA MHESHIMIWA RAIS!**

UPANDISWAJI VYEO KWA WATUMISHI:

Mheshimiwa Rais,

Katika kuhakikisha kuwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - TAKUKURU inatekeleza majukumu yake ipasavyo, mwaka wa Fedha 2019/2020, Serikali unayoiongoza **Mheshimiwa Rais**, iliwezesha TAKUKURU kupandisha vyeo watumishi wapatao **1,755**. Idadi hii ni kubwa zaidi kuwahi kutokea ndani ya chombo hiki tangu kuanzishwa kwake mwaka 1975.

Aidha, kumbukumbu za kiutumishi zinaonyesha kuwa mwaka wa fedha 2013/2014 ndio ilikuwa mara ya mwisho kwa Taasisi hii kupandisha vyeo watumishi wake. **TUNAKUSHUKURU SANA!**

UFUNGUZI WA OFISI 21 ZA WILAYA MPYA:

Mheshimiwa Rais,

Katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 Serikali iliipatia TAKUKURU fedha kiasi cha shilingi **Bilioni 5.4** (5,432,665,400) kwa lengo la kufungua ofisi 21 za TAKUKURU zilizoko katika maeneo mapya ya utawala yaliyoanzishwa.

Fedha hizo zilijumuisha kodi ya pango, samani, uhamisho wa watumishi, ujenzi wa miundombinu wezeshi (vifaa vya uchunguzi na tehama) pamoja na fedha za uendeshaji wa ofisi hizo kwa kipindi cha mwaka mzima.

TUNAKUSHUKURU SANA MHESHIMIWA RAIS, kwani ofisi zote **21** kwa sasa zinafanya kazi ya kupambana na rushwa katika wilaya hizo mpya.

Vilevile Mheshimiwa Rais tunakushukuru sana kwakuwa katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2019/ 2020 tumepitishiwa fedha kiasi cha Shilingi **Bilioni 1.5** kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya TAKUKURU wilaya za Momba, Chato, Wangingo'mbe, Mbarali pamoja na Kilolo. Pia katika mwaka huu wa fedha wa 2020/ 2021 tunatarajia kujenga ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Morogoro.
TUNAKUSHUKURU SANA MHESHIMIWA RAIS!

JENGO LA TAKUKURU MAKAO MAKUU:

Mheshimiwa Rais,

Katika kuhakikisha kuwa TAKUKURU inapata jengo kubwa kwa ajili ya ofisi zake za Makao Makuu, tayari umetupatia eneo la kujenga ofisi za TAKUKURU MAKAO MAKUU lenye ukubwa wa **Square Meter 5,547** pamoja na fedha kiasi cha **Shilingi Bilioni 1** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo hilo hapa jijini Dodoma.

Mheshimiwa Rais,

Tumeshapata Mshauri Elekezi ambaye ameandaa na kuwasilisha michoro ya Jengo la TAKUKURU Makao Makuu na pia wameshaandaa makadirio ya ujenzi – yaani Bill of Quantities.

Kwa sasa **Mheshimiwa Rais**, tunasubiri fedha za bajeti nzima ya ujenzi wa jengo hilo la Makao Makuu ili tuendelee na ujenzi na kulikamilisha jengo hilo kwa wakati.

TUNASEMA ASANTE SANA MHESHIMIWA RAIS!

OPERESHENI ZA KIUCHUNGUZI:

Mheshimiwa Rais,

Tunakushukuru pia kwa kutupatia rasilimali fedha pamoja na vitendea kazi ambavyo vimeiwezesha TAKUKURU kuendesha operesheni zake nyingi za kiuchunguzi. Operesheni hizo zimewezesha kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yetu ikiwa ni pamoja na kuongeza imani ya wananchi kwa Serikali yao.

TUNAKUSHUKURU SANA!

Mheshimiwa Rais,

Mambo yote haya uliyoyafanya na unayoendelea kuwafanyia watazania ni heshima kubwa sana kwetu TAKUKURU na ni ushahidi thabiti unaothibitisha utashi wako usio na mashaka katika kuliongoza Taifa katika kupambana na Rushwa.

Watazania tunashuhudia jitihada zako zinazo akisi dhamira yako ya kupambana na rushwa ambayo uliionyesha tangu mwanzo wa uongozi wako.

Tangu ulipoingia madarakani ulieleza wazi kwamba bila ya kupambana na rushwa hatutakuwa na maendeleo, pale uliposema wakati ukizindua Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siku ya tarehe 20 Novemba 2015:- **Ninanukuu**

Vitendo vya rushwa na ufisadi vinawanyima haki wananchi na kuitia hasara Serikali kwa mamilioni ya fedha ambazo zingeweza kutumika kwa ajili ya kujenga miradi ya maendeleo kwa ajili ya watu wetu..

Hatimaye ukaahidi mbele ya Bunge na Wananchi kwa ujumla kwa kusema kwamba:- **Ninanukuu**

Mheshimiwa Spika; Mimi nimewaahidi wananchi na nataka niirejee ahadi yangu kwao mbele ya Bunge lako tukufu, kwamba nitapambana na rushwa na ufisadi bila kigugumizi na bila haya yoyote.

Haukuishia hapo **Mheshimiwa Rais**, bali ukaendelea kuonesha chuki yako kwa watu wanaojihusisha na vitendo vya rushwa pale uliposema kwamba: **Ninanukuu:**

Mheshimiwa Spika; Wananchi wanachukia sana rushwa na ufisadi, na wamechoshwa na vitendo hivyo. Mimi pia ninachukia rushwa na ufisadi. Sifurahishwi kabisa na vitendo vya rushwa na ufisadi vinavyoendelea hapa nchini.

Mheshimiwa Rais

Dhamira yako ya kupambana na vitendo vya rushwa ni kubwa kwa sababu unatamani kuiona nchi inafanikiwa kimaendeleo kama ilivyo bainishwa kwenye Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo inaelekeza Serikali kuhakikisha kuwa inaleta maendeleo endelevu kwa wananchi. Tamaa yako hiyo uliionesha mbele ya Bunge la 11 na mbele ya Watanzania pale uliposema: **Ninanukuu:**

"Tamaa yangu na kwa kweli jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano, zitakuwa katika ujenzi wa uchumi wa kipato cha kati ambapo sura na maisha ya watanzania walio wengi yafananefanane na nchi ya kipato cha kati. Na njia mojawapo ya kutufikisha huko ni uendelezaji wa viwanda"

Mheshimiwa Rais

Dhamira hii ndiyo iliyolifikisha Taifa letu miongoni mwa Mataifa mengine kuingia katika Uchumi wa Kati hata kabla ya mwaka 2025 ambao ulikuwa umekadiriwa. **TUNAKUPONGEZA SANA MHESHIMIWA RAIS.**

Mheshimiwa Rais,

Kila mtanzania ni shahidi kuhusu mafanikio ambayo yanajitokeza kutokana na jitihada zako za kupambana na watu wanaojihusisha na vitendo vya rushwa.

Tunashuhudia jitihada kubwa ukizielekeza kwenye mipango ya kuwaletea wataanzania maendeleo na ustawi katika nyanja zote za maisha yao. Baadhi ya viashiria vya mafanikio hayo ni:

- Imani ya Wananchi kwa utendaji wa Serikali imeongezeka
- Nidhamu ya Watumishi kwenye utumishi wa umma imeongezeka na kuimarika
- Udhhibiti wa matumizi ya fedha za umma umeongezeka
- Usimamizi wa Sheria umeongezeka na kuimarika
- Uwajibikaji katika kutekeleza miradi ya maendeleo umeongezeka **na vilevile**
- Utoaji wa huduma kama za afya, elimu, miundombinu ya maji, na barabara nayo imeimarika.

TUNAKUPONGEZA SANA MHESHIMIWA RAIS.

MAHITAJI YA TAKUKURU:

Mheshimiwa Rais,

Kwa kuwa wewe ndiye Jemedari wetu na leo upo pamoja nasi hapa, kwa unyenyekevu mkubwa tunaomba tueleze **mahitaji machache** ambayo tunayahitaji katika kuimarisha jukumu letu la kuwa chombo kinachoongoza mapambano dhidi ya rushwa hapa nchini.

HALI YA MAJENGO YA OFISI ZA TAKUKURU

Mheshimiwa Rais,

Pamoja na kufanikiwa kujenga majengo haya saba ya ofisi za TAKUKURU Wilaya, bado tunakabiliwa na **Uhaba wa majengo ya kudumu ya ofisi za TAKUKURU.**

Mheshimiwa Rais,

TAKUKURU ina jumla ya ofisi **28 za Mkoa** na ofisi **117 za wilaya.** Hata hivyo hadi kufikia leo hii TAKUKURU inamiliki majengo yake ya kudumu **22 ya ofisi za Mkoa** na **22 ya ofisi za wilaya** - wakati mahitaji halisi ni **majengo 28 kwa ofisi za Mkoa** na majengo **117 kwa ofisi za wilaya.**

Mheshimiwa Rais,

Kupitia kwa Waziri wetu wa Nchi - Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, **Mhe. Kapt Mstaafu George Mkuchika,** tayari tumewasilisha maombi ya kuendelea kupatiwa fedha za kujenga majengo yetu lakini pia wakati tukisubiri ujenzi, tunaomba katika maeneo ambapo kuna majengo ya Serikali, basi viongozi wa eneo husika watupatie TAKUKURU majengo hayo ili tuweze kuwa na ofisi inayojitegemea ya kushughulikia masuala ya kuzuia na kupambana na rushwa.

FEDHA ZA KUKAMILISHA MAJENGO SABA YA OFISI ZA WILAYA:

Mheshimiwa Rais,

Hadi kufikia hatua ya uzinduzi wa majengo haya ya TAKUKURU Wilaya, kila jengo linakadiriwa kugharimu takriban **Shilingi Milioni 143**. Gharama hii ni kwa matumizi ya ujenzi wa jengo la ofisi tu na haikujumuisha mahitajio mengine ya ofisi ambayo ni pamoja na Uzio na Samani za ofisi.

Mheshimiwa Rais,

Gharama ya ujenzi wa uzio wa ofisi hizi pamoja na samani haikujumuishwa kwani tungefanya hivyo ujenzi huu ungetugaribu zaidi ya **shilingi Bilioni moja**.

Kwa makadirio, kila jengo linatakiwa lijengewe uzio wa urefu wa **mita 354** kwani ukubwa wa maeneo ya ofisi hizi kwa kila moja ni takriban **Square Metre 7,800**. Hivyo, kwa makadirio hayo, kwa majengo saba tungelihitaji uzio wa urefu wa **mita 2,478** ambazo gharama yake ni takriban shilingi **Milioni 495**. **Mheshimiwa Rais**, kiasi hiki cha fedha tayari kingetumia nusu ya zile fedha (Shilingi Bilioni 1) ambazo tulikuwa tumepewa kwa ajili ya ujenzi wa majengo haya saba.

Kama tunavyofahamu **Mheshimiwa Rais**, ujenzi wa uzio wa ofisi pamoja na ununuzi wa samani za ofisi ni muhimu ili kukamilisha majengo haya ambayo yamekusudiwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu nyeti kama ya TAKUKURU.

Kutokana na sababu hiyo **Mheshimiwa Rais** tunaomba tuongezewe fedha kiasi cha **shilingi Bilioni 1**, ili tuweze kukamilisha ujenzi wa uzio wa majengo hayo saba pamoja na kununua samani kwa matumizi ya ofisi hizo.

NYUMBA ZA MAKAZI YA VIONGOZI NA WATUMISHI WA TAKUKURU

Mheshimiwa Rais

Pamoja na ukweli kuwa umetupatia fedha za ujenzi wa jengo la ofisi ya TAKUKURU Makao Makuu, tunakuomba utufikirie kutupatia fedha za kuweza kujenga nyumba za kuishi Wakuu wa TAKUKURU katika Mikoa na Wilaya na ikiwezekana pia tuweze kuwa na nyumba za makazi kwa ajili ya watumishi.

Tunatambua kuwa ujenzi huo unaweza kugharimu fedha nyingi hata hivyo tupo tayari kuanza ujenzi wa majengo hayo kwa awamu na tayari TAKUKURU tunavyo jumla ya **viwanja 156** nchi nzima ambavyo havina majengo.

Mheshimiwa Rais,

Tunaleta ombi la majengo ya makazi ya watumishi kutokana na changamoto ambayo imekuwa ikiwakabili watumishi wa TAKUKURU wanapokuwa mikoani au wilayani na kulazimika kutafuta nyumba za kupanga kwa ajili ya makazi yao.

Uzoefu wetu unaonesha kuwa mara zote imekuwa ni shida sana kwa watumishi wa TAKUKURU kupata nyumba za kupanga kutokana na kwamba wao wanaonekana kuwa wataishia kuwachunguza wenye nyumba pamoja na majirani zao.

VIWANJA VYA WATUMISHI WALIOTAPELIWA:

Mheshimiwa Rais

Watumishi wa TAKUKURU wanakumbuka kwamba aliyekuwa Mkurugenzi wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathimini wa TAKUKURU, Bi. Kulthum Mansoor amefikishwa mahakamani kwa makosa kadhaa yakiwemo makosa ya kuwarubuni baadhi ya watumishi wa TAKUKURU kwamba angewauzia viwanja kwa utaratibu wa kumlipa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Rais,

Ardhi ambayo watumishi walikuwa wauziwe ni shamba Nambari 126 la Nzole lililoko Bagamoyo mkoani Pwani.

Uchunguzi wetu umebaini kwamba, kwa mujibu wa kumbukumbu za Wizara ya Ardhi mpaka kufikia mwezi Julai 2020, shamba hilo namba 126 la Nzole lilisha rejeshwa Serikalini na liko mbioni kupimwa ili wananchi wapatiwe miliki. Kwa maana hiyo, **shamba hilo linabaki kuwa chini ya mamlaka yako Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Vilevile, tunatambua kwamba, Ndugu Kulthumu anafanya utaratibu na Ofisi ya Mwendesha Mashitaka wa kurejesha fedha Serikalini kwa utaratibu wa ***Plea Bargaining*** ambapo kwa utaratibu huo watumishi hawatapata chochote kwa maana hela hiyo itarejeshwa Serikalini.

Ni kwa msingi huo **Mheshimiwa Rais,** kwa mamlaka uliyonayo, tunakuomba eneo hili lipimwe na kugawiwa viwanja hivyo kwa watumishi waliotapeliwa na mtumishi huyo mwenzetu. Kitendo hicho **Mheshimiwa Rais,** kitaongeza morali ya watumishi hao na pia kitawaondolea adha ya kutapeliwa fedha zao.

UCHAGUZI MKUU WA VIONGOZI – OKTOBA 2020:

Mheshimiwa Rais,

Mwaka huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu wa viongozi kwa ngazi ya Diwani, Wabunge pamoja na Rais.

Kwa kutambua umuhimu wa wataanzania kuchagua viongozi walio BORA, WAADILIFU na WASIOJIHUSISHA NA VITENDO VYA RUSHWA, TAKUKURU nchi nzima tumejipanga vema ili kuhakikisha tunaendelea kuelimisha jamii juu ya MADHARA YA RUSHWA KATIKA UCHAGUZI.

Katika kusesitiza jambo hili, nilitoa RAI kupitia vyombo vya habari na kuwatahadharisha wale wote wenye nia ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2020, kuhakikisha kuwa hawata jihusisha kabisa na vitendo vitakavyokuwa na viashiria vya rushwa. Lengo la TAKUKURU ni kuhakikisha kwamba tunafanya uchaguzi ulio huru na wa haki na tunatamani tuwe na uchaguzi ambao hautagubikwa na vitendo vya rushwa.

Ninatoa wito tena kwa watazania kwamba wajiepushe na vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi na mtu yeyote atakayejihusisha na vitendo hivyo atakutana na mkono wa sheria na ataadhibiwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria.

HITIMISHO

Mheshimiwa Rais,

Niliona ni fursa kutumia nafasi hii adhimu kueleza haya machache kwani tukio hili la wewe **Mheshimiwa Rais** kushiriki nasi katika kutuzindulia majengo yetu saba NI LA KIHISTORIA. **TUNAKUSHUKURU SANA!**

Mheshimiwa Rais,

Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Kapt (Mst) George H. Mkuchika (MB), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na

Mheshimiwa Dkt Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora - kwa namna ambavyo wamekuwa wakishirikiana nasi katika kila matukio yanayohusu mapambano dhidi ya rushwa.

Hii inatuonyesha dhamira ya dhati waliyonayo katika kusimamia mapambano dhidi ya rushwa hapa nchni. **TUNAWASHUKURU SANA!**

Tunaendelea kuwasihi wananchi waendeleo kukuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu - Dkt John Pombe Joseph Magufuli ambaye siku zote umekuwa mstari wa mbele katika kuongoza mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Rais,

Baada ya maelezo hayo ninaomba sasa nimkaribishe Mhe. George Simbachawene, Waziri wa Mambo ya Ndani, ili aweze kutoa salamu zake na hatimaye akukaribishe ili uzungumze nasi pamoja na kutuzindulia majengo yetu.

Mheshimiwa Waziri. KARIBU.